

KESI

 Katika Marko, mlango wa 16, tukianza na kifungu cha 9, ningependa kusoma. Fungu lenye utukufu, linahusu ufufuo.

Naye Yesu alipofufuka alfajiri siku ya kwanza ya juma, alimtokea kwanza Mariamu Magdalene, ambaye kwanza alimtoa pepo saba.

Huyo akashika njia akawapasha habari wale waliokuwa pamoja naye, nao wakali wanaomboleza na kulia.

Walakini hao waliposikia kama yu hai, na ameona . . . naye amemwona, hawakusadiki.

Baada ya hayo akawatokea watu wawili miongoni mwao, ana sura nyingine; nao walikuwa wakishika njia kwenda shamba.

Na hao wakaenda zao wakawapa habari wale wengine; wala hao hawakuwasadiki.

Baadaye, akaonekana na wale kumi na mmoja walipokuwa wakila, akawakemea kwa kutokuamini kwao na ugumu wa mioyo yao, kwa kuwa hawakuwasadiki wale waliomwona alipofufuka katika wafu.

Akawaambia, Enendeni ulimwenguni mwote, mkaihubiri Injili kwa kila kiumbe.

Aaminiye na kubatizwa ataokoka; asiyeamini, atahukumiwa.

Na ishara hizi zitafuatana na hao waaminio; kwa jina langu watatoa pepo; watasema kwa lugha mpya;

Watahika nyoka; hata wakinywa kitu cha kufisha, hakitawadhuru kabisa; wataweka mikono yao juu ya wagonjwa, nao watapata afya.

Basi Bwana Yesu, baada ya kusema nao, akachukuliwa juu mbinguni, akaketi mkono wa kuume wa Mungu.

Nao wale wakatoka, wakahubiri kotekote, Bwana akitenda kazi pamoja nao, . . . kulithibitisha lile neno kwa ishara zilizofuatana nalo. Amina.

² Hebu na tuombe. Bwana Yesu, tunasema sasa, tunapokaribia Kiti cha Enzi cha Baba. Na katika Jina Lako, tunaamini hili kuwa ni Neno Lako. Tunaamini hili kuwa ni Maneno ya mwisho yaliyotoka midomoni Mwako kabla ya Wewe kupaa juu. Nasi tunaomba ya kwamba utayabariki kwa mioyo yetu alasiri hii,

kwa ajili ya wale walio wagonjwa. Tunakushukuru kwa kuita idadi kubwa kwenye kiti Chako cha Enzi usiku uliopita, nasi tuliona ile mistari mikubwa ya wale watu, wanaume, wanawake, kina baba, watoto, kina mama, wakishuka kwenye safu na kuingia katika chumba cha maombi. Tunakushukuru kwa hilo, Baba. Na sasa tunaomba ya kwamba utawapatia utajiri wa Ufalme Wako, na hebu kuwe na imani miongoni mwetu alasiri ya leo kulifanya Neno la Mungu kuwa halisi kwetu. Na Wewe ndiye wa pekee awezaye kutenda hili, Baba, kwa hiyo tunaomba hayo katika Jina la Yesu Kristo. Amina.

Mwaweza kuketi.

³ Sasa somo langu alasiri ya leo, ninataka kulichukua, nalo kidogo linasikika lisilo kawaida. Nami nataka kulichukua kwa sababu jana, kwenye kiamshakinywa, nilikutana na mmoja wa watu wazuri sana, naye ameketi nyuma yangu sasa, wakili. Na tulikuwa tukizungumza juu ya kesi, na kwa namna fulani ilikuwa ni kesi ya dhihaka, ama kitu fulani, aliyofanyiwa Bwana wetu. Nami ni—ninaamini kwa hakika ya kwamba mtu huyo angefaa zaidi kusimama hapa na kuifananiisha na mahakama za nchi, kwa sababu nimenena habari zake tangu nilipokutana naye, na yeye. . . Wananambia kuwa yeye ni wakili mzuri sana, kwa hiyo ninajua angemfanyia kesi ya haki. Na kwa kuwa Yesu hakufanyiwa aina ya kesi ifaayo. . . Na Yeye ni Neno. Sote tunakubaliana juu ya hilo. Yeye ni Neno. Basi nimesoma Neno Lake, na tutalifanyia Neno kesi alasiri ya leo.

Neno linafanyiwa kesi.

⁴ Kesi ni, ahadi za Neno la Mungu dhidi ya ulimwengu. Na chanzo cha shtaka, ni, kukiuka ahadi. Na ninii. . . Nafikiri wakili mwendesha mashtaka sikuzote huiwakilisha serikali. Nafikiri hiyo ni sahihi. Na ninii. . . Shetani ndiye wakili mwendesha mashtaka, anauwakilisha ulimwengu, katika kesi hii. Naye Mshtakiwa ni Mungu. Naye Shahidi wa Mshtakiwa ni Roho Mtakatifu. Hivyo nataka kulifanya kanisa, kusanyiko, kuwa wazee wa mahakama na pia hakimumu. Na hebu tuisikilize kesi sasa, tunapoondoa pazia jukwaani na kuona mahali tunapoketi.

⁵ Sasa, msisahau sasa, kwamba ninii—ninii. . . kile tunachoona hapa ndicho chanzo cha kesi hii, ni, Neno la Mungu dhidi ya ulimwengu. Sababu ya shtaka, ni, kukiuka ahadi, yaani, kwamba ulimwengu unadai kuwa Mungu alifanya ahadi ambayo si kweli. Huko ni kukiukwa kwa ahadi, “Yeye hatimizi ahadi Yake.” Na wakili mwendesha mashtaka katika kesi hii ni Shetani, anayewakilisha ulimwengu. Naye Mshtakiwa ni Mungu Mwenyewe. Naye Shahidi wa Mshtakiwa ni Roho Mtakatifu.

Basi sasa tunaitisha utulivu mahakamani.

⁶ Na sasa wakili mwendesha mashtaka atamwita shahidi wake wa kwanza asimame apate kumwapisha. Na, sasa, anao mashahidi watatu alasiri ya leo ambao ninataka kuwatumia,

anaotaka kuwatumia, hasa, katika kesi hii. Nao mashahidi hawa ni Bw. Asiyeamini, anayefuata ni Bw. Mwenye Kushuku, na anayefuata atakayeitwa atakuwa Bw. Kukosa Subira. Sasa, hawa ndio mashahidi dhidi ya kesi, kwamba, “Mungu hatimizi Neno Lake. Neno Lake si kweli.”

⁷ Na tunaweza kuona, kabla hatujaanzisha kesi, kwamba—kwamba wengi sana wa ulimwenguni hujaribu kusema ya kwamba Neno la Mungu si kweli. Kwa mfano, hili nilisoma tu, nilikuwa nikisoma marejeo chini ya ukurasa kwenye Scofield. Nami nilikuwa nikiwazia hadithi niliyosimuliwa wakati fulani. Nadhani...sidhani nimewahi kuinukuu, hasa katika mkutano huu. Lakini, kwamba m—mwanamke fulani wakati mmoja alikuwa na mvulana mdogo mzuri, yeye alitaka kuwa mhudumu. Basi kwa kiasi fulani alikuwa mwanamke maskini, naye alitaka mvulana wake apate elimu yote nzuri na mafunzo aliyoweza (ambayo, mama yeyote yule angemtaka mvulana wake, kama aliitiwa jambo kama hilo), yengekuwa mafunzo yaliyo bora kuliko yote yaliyoweza kupatikana, kwa nini, alimtaka ayapate. Kwa hiyo alimpeleka kwenye seminari nzuri kuliko zote za kidini aliyojua pa kumpeleka.

⁸ Vema, alikuwa amekuwa pale kwa yapata mwaka mmoja, ndipo siku moja mama yake akashikwa na ugonjwa mbaya sana, kwa kweli alikuwa katika hali mbaya sana. Na—nao waliendelea kupiga simu na kutuma ujumbe wa telegramu. Alikuwa anaishi peke yake. Kusudi aweze kuitwa nyumbani kwa sababu alishikwa na mafua makali sana, na yakaishia kuwa nimonia maradufu, na alikuwa na msongamano kwenye ninii... wa mapafu, na alikuwa anangojea kufa. Moyo wake ulionekana kuwa mbaya sana. Kwa hiyo daktari huyo mwaminifu alikuwa anafanya yote aliyojua, kuyaokoa maisha ya mwanamke huyo, naye alizidi kudhoofika siku zote. Hivyo basi da—daktari alituma ujumbe wa telegramu kwa kijana huyo, na akasema, “Jiandae mara moja. Fanya maandalizi ya nafasi yako kwenye ndege, ambapo huenda ikakubidi kuja kwa mama yako wakati wote, kwa sababu anaonekana kuwa amekaribia sana mauti.” Na kisha mvulana huyo, akiwa amefadhaika mno, aliziweka nguo zake tayari na alikuwa anajiandaa kupanda ndege. Ndipo—ndipo telegramu ikaja moja kwa moja kutoka kwa mamake, “Usije, mwanangu. Nilipona.”

⁹ Kwa hiyo basi yapata mwaka mmoja baadaye, ama miezi sita baadaye, naamini ndivyo ilivyokuwa, kwamba alirudi nyumbani kwake. Na baada ya kumwamkua mama yake, nao walikuwa na ushirika pamoja, akasema, “Mama, kuna swali moja ambalo lingali niani mwangu.” Kasema, “Wakati ulipokuwa mgonjwa sana,” kisha kasema, “hukuniandikia na kunielezea mambo yote. Ulisema tu kuwa ulipona, na hukunielezea yote ya jinsi hayo yalivyotukia.”

10 Akasema, “Mwanangu, unajua pale chini hapa mtaani, pale pale ambapo palikuwa na duka la vyakula pale mahali fulani?”

“Naam.”

11 “Kuna kundi la watu huko chini ambao huabudu katika jengo lile dogo.”

“Naam,” kasema, “Ninawakumbuka, wao ni wapentekoste.”

12 Kasema, “Naam, hiyo ni kweli.” Kasema, “Nilipokuwa katika hali mbaya sana,” kasema, “kuna mama mzuri aliyenijia hapa. Naye akasema, ‘Dada, tulikuwa huko chini katika mkutano wa maombi, na tukasikia ya kwamba wewe ni mgonjwa sana, nawe una mvulana huko mbali katika—katika shule ya seminari, apate kuwa mhudumu. Na wakati tulipokuwa tukiomba, Bwana alitufunulia ya kwamba tunapaswa kuja tukuombee.’ Pia kasema, ‘Vema,’” akasema, “‘hiyo, hiyo itakuwa sawa.’ Kasema, ‘Utajali ikiwa mchungaji wetu atakuja na kuomba?’ Kasema, ‘Mbona, hakika sijali, mama. Nitafurahia,’ kasema. Kwa hiyo wakamleta nanii...Daktari akasema kwamba tutakuwa sawa. Kwa hiyo mchungaji akaja, naye akasoma maandiko haya hapa katika Marko, mlango wa 16. Ndipo akasema, ‘Hili ndilo Biblia isemalo.’” Basi akaweka mikono yake juu ya mwanamke huyo na kuomba, akaondoka. Kisha kasema, yeye “alipona,” akasema.

“Loo,” akasema, “Mama!”

Akasema, “Hiyo si ni ya ajabu, mwanangu? Wazia hilo!”

13 “Loo,” akasema, “Mama, bila shaka hiyo haikuwa na uhusiano wowote na kupona kwako.” Anasema, “Labda baadhi ya dawa ambazo daktari alikuwa amekupa hapo awali, hazikufanya kazi tu kwa wakati.”

14 Kisha kasema, “Loo!” Akasema, “La, mwanangu. Daktari alikuwa ameacha kunipa dawa siku mbili, akasema hakuwa na la kufanya. Aliniweka tu chini ya oksijeni na kusema hakuwa na la kufanya. Nami nilizidi kudhoofika.”

15 “Loo,” akasema, “Mama, ha—haikuwa hiyo.” Kasema, “Unaona, hao ni watu wasioelimika.” Kasema, “Hao kwa kweli hawaelewi. Wanasoma tu Biblia.” Ndipo kasema, “Unaona?”

Akasema, “Vema, hivi hatupaswi kuiamini Biblia, mwanangu?”

16 “Loo, hakika.” Kasema, “Mama, tunapaswa kuiamini, lakini,” kasema, “unajua, huko shuleni,” kasema, “tulijifunza kwamba Hapo ambapo alisoma hapo kutoka kwenye Marko 16, kuanzia kifungu cha 9 kuendelea, hata haijavuviwa.”

“Vema,” kasema, “utukufu kwa Mungu!”

17 Akasema, “Mama, unajiadhibisha kama hao watu.” Ndipo kasema, “Mbona, wazo lenyewe!”

Akasema, “Vema, kipenzi, nilikuwa tu nikiwazia.”

Kasema, “Unawazia nini?”

¹⁸ Kasema, “Kama Mungu anaweza kuniponya na sehemu hiyo ya Neno ambayo haijavuviwa, angeweza kufanya nini na ile hasa iliyovuviwa?” Kwa hiyo, Hilo, Hilo ni... [Kusanyiko linashangilia—Mh.] Basi tunaamini imevuviwa.

¹⁹ Kwa hiyo, sasa hii, tutamruhusu mwendesha mashtaka awaite mashahidi wake, wa kwanza kizimbani, kutoa ushuhuda wa mashtaka.

²⁰ Ndiyo kwanza niseme hilo dakika chache zilizopita, kwa sababu nilikuwa tu nikisoma, nilipokuwa nikisoma kifungu hiki, Bw. Scofield anasema kwamba baadhi ya miswada haina Hiyo. Hapo labda ndipo ambapo uwongo huo ulipotokea. Lakini Hilo ni kweli.

²¹ Kwa hiyo Bw. Kutokuamini anakuja kizimbani, na kuchukua nafasi yake sasa kushuhudia dhidi ya Neno la Mungu, kulipinga. Na sasa wakati yeye... Anapaswa kuwa ndiye shahidi wa kwanza kusimama. Sasa tunaona ya kwamba akisha kuapishwa, sasa malalamishi yake ni haya, kwamba “ahadi za Neno la Mungu kwa jumla si kweli.”

²² Sasa, mashahidi hawa wote ambao mwendesha mashtaka anawaleta, wanadai kuwa ni waaminio. Wote wanadai kuwa ni waaminio, ama, wanatoa ushahidi wa hili, “Kamwe tusingehudhuria mikutano kama hiyo iwapo hatukuwa waaminio.” Kwa hiyo wa—wanasema kwamba wao ni waaminio.

²³ Na malalamishi ambayo Bw. Asiyeamini anatoa dhidi ya Neno la Mungu, anadai kwamba “Marko 16 si kweli, haliwezi kabisa kuwa kweli.” Kwani alisema kwamba alikuwa mgonjwa kwa muda fulani, naye anatoa ushuhuda wake sasa kwamba alikuwa mgonjwa kwa muda fulani, ndipo yeye “akaenda kwenye kilichodaiwa kuwa ni mkutano wa Roho Mtakatifu ambapo watu walikuwa wakiweka mikono juu ya wagonjwa, nao wakadai kuwa walikuwa wanaponywa.” Kwa hiyo akaingia kwenye mstari huu wa maombi, na alipoingia... Alikuwa ameugua sana kwa muda, naye “akaombewa na kundi hili la watu wenye Roho Mtakatifu (kilichodaiwa kuwa ni Roho Mtakatifu) waliokuwa wakipaza sauti na kupiga makelele, na kudai kuwa waliponywa.” Ndipo Bw. Asiyeamini akapitia mstari huu, akawekewa mikono, “Na hiyo ilikuwa ni zaidi ya miezi miwili iliyopita, na hakujawa hata na dalili moja ya kupona.” Kwa hiyo anasema kwamba, “Neno la Mungu, sehemu hiyo, si kweli.”

²⁴ Sasa, kwa hiyo mwendesha mashtaka anamteremsha shahidi wake wa kwanza, anampandisha shahidi wake anayefuata kwenye kizimba. Naye shahidi wa pili anayesimama, ni Bw. Mwenye Kushuku. Anaapishwa, anaingia kizimbani. Sasa, anadai kwamba yeye ni mwaminio, naye “alisikia jijini kwamba kulikuwa na kanisa ambapo walikuwa

na mchungaji mwaminifu, aliyedaiwa kuwa ni mcha Mungu, ndivyo kusanyiko lisemavyo. Naye mtu huyu aliamini maandiko, ndivyo asemavyo. Basi aliwaombea wagonjwa na kuwapaka mafuta. Ndipo akasoma mlango wa hii katika Biblia, katika Yakobo mlango wa 5, kifungu cha 14, 'Mtu wa kwenu amekuwa hawezi? Na awaite wazee wa kanisa; nao wampake mafuta, wamwombee; kule kuomba kwa imani kutamwoko mgonjwa yule, na Mungu atamwinua.'" Kwa hiyo akasema kwamba aliingia, akiwa mgonjwa, imekataa kabisa yeye kuweza kupona kutokana na homa hii ya kupanda na kushuka aliyokuwa nayo. Naye daktari alisema asingeweza kupona kutokana na hiyo, hakuna njia kwake kupona. Kwa hiyo yeye "akaamini Neno la Mungu," kisha "akampata huyu anayedaiwa kuwa ni mchungaji mcha Mungu," ambaye kusanyiko lote lilikuwa na kila aina za shuhuda ati walikuwa wameponywa, na kadhalika. Ndipo mchungaji huyu mcha Mungu akamwombee, akimpaka mafuta, kulingana na Neno la Mungu. Hakutilia shaka uaminifu wa mtu huyo, hakutilia shaka uaminifu wa kusanyiko; bali mchungaji alitimiza utaratibu kama tu Biblia isemavyo, akampaka mafuta na kumwombee. "Na hiyo ilikuwa zaidi ya miezi sita iliyopita," naye "hajaonyesha hata dalili moja ya kupona." Basi anatoa ushuhuda huo. Sasa shahidi wa pili anashuka chini.

²⁵ Basi mwendesha mashtaka anamleta shahidi wake mwingine, ambaye ni Bw. Mkosa Subira. Anamleta kisha anaapishwa, kutoa ushuhuda dhidi ya Neno la Mungu, kuwa si kweli. Mtu huyu anakuja na anadai kuwa yeye ni mwaminio, na alikuwa akisoma siku moja katika Marko, mlango wa 16, ama mlango wa 11 wa Marko, hasa, na kuanzia kifungu cha 22, ambapo Yesu Mwenyewe... Anadai kuwa yeye "alikuwa na Biblia yenye herufi nyekundu, na hizo herufi nyekundu zilikuwa ndizo Maneno hasa aliyosema Yesu, Mwenyewe. Na kwamba katika Biblia hii yenye herufi nyekundu, katika Marko, mlango wa 11, ambapo Yesu alikuwa akinena, alitamka nukuu hii, 'Mwaminini Mungu. Kwa maana amin, amin, nawaambia, ukiuambia mlima huu "ukatupwe baharini," wala usione shaka, ila uamini kwamba hayo uliyosema yatatimia, yatakuwa yako.'" Naye "alikuwa kiwete," anasema hapa, "kwa—kwa miaka mingi," tangu alipokuwa mvulana. Alikuwa amelemaa miguu yake. Ilimbidi kutembea kwa magongo. Kwa hiyo alikubali hilo kuwa ni Neno la Mungu lisilokosea, naye akasema ndani ya moyo wake, kama anavyodai, kushuhudia sasa, akasema, "Nitatembea." Na akakubali Neno la Yesu Kristo, alisema kwamba atatembea kwa sababu Yesu alisema hivyo. "Ukiuambia mlima huu 'ng'oka,' na ukiamini, mwombapo, aminini ya kwamba mnapokea yale mwombayo, nayo yatakuwa yenu." Naye aliomba huo, aliuomba, akasema yeye "ataupokea, na hiyo ni miaka mitano iliyopita." Naye angali amelemaa kwenye miguu yake, hajapata mabadiliko yoyote.

²⁶ Sasa mwendesha mashtaka anakuja baada ya mashahidi wake kutoa nukuu tatu mbalimbali za Maandiko (ambayo ni ninii, katika mahakama za Kiyahudi, ni ushahidi), wametoa shuhuda tatu za Maandiko yaliyoandikwa katika Biblia ya Mungu, “inayodhaniwa kuwa Yesu Kristo alisema Hayo,” ambaye ni Mwana wa Mungu, Mungu aliyefanyika mwili, akikaa ndani ya Mtu, kutokosea. Ndipo mwendesha mashtaka anakuja sasa kuwakazieni kesi hiyo enyi watu.

Sasa, kumbukeni, ninyi ndio wazee wa mahakama nanyi ndio hakimumu.

²⁷ Kwa hiyo mwendesha mashtaka anataka mjue sasa, anapoikaza kesi hii tena, watu hawa wanadai kuwa ni waaminio kama tu wengine wote wanavyodai. Basi anadai pia, mwendesha mashtaka anataka mjue kwamba “Mungu hana haki ya kuweka ahadi za kijinga hivi katika Neno Lake, wakati Yeye haziungi mkono, kwa kuwa anawapa watoto Wake waaminio kutangaza. Na kwa wao kulitangaza, wanaaibishwa na kufedheheshwa, kwa kuyatangaza Maneno yasiyo kweli.” Mwendesha mashtaka sasa, “Kwa sababu ameshindwa kutimiza ahadi za mashahidi hawa watatu, ambazo zinatekelezwa kabisa kulingana na Neno la Mungu.” Naye anataka, mwendesha mashtaka anataka mjue kwamba “Mungu ameshindwa, katika visa vyote vitatu, kufanya madhihirisho yoyote ya kudumisha Neno Lake” (anaikaza kwa ajili yenu), “na kwa hawa wanaojidai kuwa ni waaminio.”

²⁸ Halafu tena, mwendesha mashtaka anataka kugeuka, kuvuta usikivu wenu kwa jambo jingine. “Yeye, yaani Mungu, aliahidi kwamba yote yanawezekana kwa wale waaminio. Aliahidi hilo.” Mwendesha mashtaka anataka mjue hilo. “Na hawa wanaojiita waaminio wamejaribu kulidumisha Neno hili, na Yeye ameshindwa kulidumisha, kwa hivyo ameshtakiwa kwa kukiuka ahadi.”

²⁹ Bado tena, mwendesha mashtaka anataka kuvuta usikivu wenu kwa Neno jingine la Mungu. “Yeye anadai kuwa hai baada ya kifo Chake. Yesu anadai kuwa hai baada ya kifo Chake.” Tena mwendesha mashtaka anataka mjue kwamba yeye “hajaona Mtu aliye na alama za misumari mikononi Mwake, na makovu kote mwilini Mwake kuanzia kope, na alama za misumari miguuni Mwake.” Wala hajapata “kuona taji ya miiba juu ya kichwa cha Mtu yeyote. Na hata hivyo anadai kuwa hai baada ya kifo Chake. Pia Yeye anadai, kwamba katika Waebrania 13:8, ati yu hai. Na hiyo si kweli. Yeye anadai pia, katika mlango wa Luka, mlango wa 17 na kifungu cha 30, kwamba katika siku hizi tunazoishi sasa, ati angejifunua Mwenyewe; kama alivyokuwa wakati ule, ndivyo atakavyokuwa. Anadai vile vile,” mwendesha mashtaka sasa akiwatolea kesi iliyotiliwa mkazo, “kwamba katika Ufunuo 10, kwamba malaika wa saba, atakapopiga baragumu yake” (huyo ni ma—malaika kwa kanisa la Laodikia, anayepaswa kuliita kanisa lirudi kwenye Imani ya kina baba), “kwamba

malaika huyu akipiga baragumu yake, kwamba siri zote za Mungu zinapaswa kufunuliwa katika siku hiyo. Pia anadai, kwamba katika Malaki 4, ati manabii watakatifu walitabiri kwamba kutakuwako nabii atakayetokea katika siku hiyo, kuyafanya madai haya kuwa kweli. Na hakuna moja la Hili lililo kweli! Pia anadai ya kwamba mbingu na nchi zitashindwa, bali Neno Lake halitapita kamwe.”

³⁰ Sasa mwendesha mashtaka anayo kesi hapa. Anaikaza kwelikweli. Sasa anaikabidhi kwenu enyi wasikilizaji, kwenu mlio hakimu na pia wazee wa mahakama. Sasa tumesikia upande wake, tumewasikiliza mashahidi. Tumesikia waliyosema kuhusu Hilo. Tumesikia yale mwendesha mashtaka aliyomiminia, Neno, na kuikaza kutoka pande zote, “Ahadi zote alizotoa Mungu, wala hakuna hata moja ya hizo” awezayo kuiona “kwamba ni Kweli.” Kwa hiyo anajaribu kuleta shtaka dhidi ya Mungu, na dhidi “Yake kutoa ahadi za kijinga kama hizo, kwa sababu ahadi alizotoa Mungu ni za kijinga kabisa. Ahadi alizofanya kwa ajili ya siku hii ni za kijinga kabisa. Wala hatimizi Hizo!” Sasa tumesikia upande wake, basi sasa hebu tuwaulize mashahidi wa mwendesha mashtaka waketi, na mwendesha mashtaka.

³¹ Na sasa tutamwita Shahidi wa Utetezi kwa Mtetezi. Na Shahidi wa Utetezi sasa ni Roho Mtakatifu, sasa Yeye anakuja na kusimama kumtetea Mshtakiwa. Sasa, jambo la kwanza analotaka kuijulisha mahakama hii, haleluya, ya kwamba mwendesha mashtaka analifasiri Neno vibaya kwa watu, vile tu alivyofanya kwa Hawa pale mwanzo. Kumbukeni, alikuwa ndiye mfasiri wake. Mungu alisema waliyopaswa kufanya, na hakungekuwako na mauti, huzuni wala chochote, naye alikuja na kulifasiri Neno visivyo. Hivyo basi mwanadamu alipoondoka nyuma ya Neno la Mungu, hiyo inawafanya kitu gani? Halindwi na Mungu. Lakini, mnaona, Shetani ndiye aliyekuwa mfasiri wa Neno kwa Hawa. Asingemsikiliza mumewe na Mungu, bali alichukua fasiri ya mwendesha mashtaka ya Neno. Naye hana haki kutoa fasiri, wala mtu yeyote. Mungu Ndiye anayejifasiria Mwenyewe. Hatuhitaji; Yeye hulitimiza Neno Lake, tunaamini. Sasa anataka kuvuta usikivu wenu kwa jambo hilo, ya kwamba mfasiri yule yule wa Maneno ya kwanza ya Mungu yaliyonenwa, ndiye mwendesha mashtaka anayejaribu ku—kuleta shtaka mbele ya mahakama hii alasiri ya leo, wa yule yule, naye amelifasiri neno vibaya. Hilo ndilo jambo la kwanza Shahidi wa Utetezi analotaka kusema. Sasa, alitaka kuwajulisha hili, kwamba yeye alikuwa ni mfasiri wa Hawa naye alilifasiri Neno vibaya.

³² Jambo la kwanza, Yeye anataka kuwapa wazo hili, ya kwamba ahadi ni kwa waaminio pekee; sio wanaojisingizia imani, wenye kushuku, ama wasioamini. Ni kwa wale tu wanaoamini! Sasa anaitaka mahakama hii...Shahidi wa

Utetezi (Roho Mtakatifu) anaitaka mahakama hii itambue ya kwamba ahadi hizi ni kwa ajili ya waaminio pekee.

Halafu swali la udadisi, alisema, “Hawa ni waaminio!”

³³ Na sasa Shahidi wa Utetezi Mwenyewe yafaa ajue kama hao ni waaminio au la, kwa sababu Yeye Ndiye ahuishaye ahadi. Sasa utarukaje hilo? Ana ninii nyingi. . .kesi kali inaendelea. Utarukaje hilo? Roho Mtakatifu anafaa kujua, kwani Yeye ndiye Uhai uliomo ndani ya Neno, Yeye Ndiye hulihuisha Neno. Kama tu ambavyo roho yako huuhuisha mwili wako, nao mwili unahuishwa na roho; pasipo roho, mwili haujiwezi, mwili umekufa. Nalo Neno limekufa bila Roho. Inahitaji Roho kulileta Neno, kulifanya hai. Naye ndiye Mwenye Kuhuisha Neno hilo, na Yeye ndiye Shahidi Mtetezi wa Mshtakiwa. Amina. Utarukaje hilo? Ninaitaka mahakama hii ifahamu hilo vizuri sana, kwamba Yeye ndiye Mwenye Kuhuisha, Yeye anafaa kujua. Yeye hulihuisha Neno.

³⁴ Tena, anataka kuvuta usikivu wa mahakama hii kwenye Neno la ahadi linalojadiliwa. Kamwe hakuwawekea muda maalum kwao kupona. Yeye alisema, “Kule kuomba kwa imani kutamwoko mgonjwa yule, na Mungu atamwinua.” Hakusema, “papo hapo.” “Wataweka mikono juu ya wagonjwa, nao watapata afya.” Kamwe hakusema, “siku moja, mwezi, mwaka.” Yeye alisema tu, “Watapata!” Shahidi wa Utetezi anawatakeni mjue hilo, kwamba Yeye hakusema kutafanyika muujiza. Yeye alisema tu, “Watapata afya!” Lifasiri Neno vizuri. “Watapata afya.” Kamwe hakuweka muda maalum. Na, hiyo ni, ikiwa wao ni waaminio! Ikiwa wao ni waaminio, utapona. “Wataweka mikono juu ya wagonjwa, nao watapata afya,” iwe ni sasa, juma moja, mwezi, mwaka, miaka kumi, miaka ishirini, miaka hamsini. “Watapata afya.” Alisema hivyo! Hiyo ni, ikiwa wanaweza kushikilia kuamini kwao. Sasa, huyo ndiye Shahidi wa Utetezi.

³⁵ Kitu kingine, Shahidi wa Utetezi anataka kuvuta usikivu wa mahakama hii alasiri ya leo ya kwamba, pia, Neno ni Mbegu, nayo Mbegu haina budi kuanguka kwenye udongo wenye rutuba ili kuihuisha. Mbegu haitakua juu ya mwamba. Mbegu haina budi kuwa na rutuba. Nalo Neno halina budi kuanguka kwenye imani, ambayo ndiyo rutuba ambayo hufanya Neno litimie. Sasa Shahidi wa Utetezi wakati huu. . .

³⁶ Tungeweza kuita wengi zaidi, mambo yangeweza kutajwa. Bali, hatutaki kuwawekea muda mrefu kupita kiasi, tuna mstari mkubwa wa maombi. Ninawatakeni, enyi mahakama, kusikiliza.

³⁷ Shahidi wa Utetezi sasa atamwita shahidi Wake. Mnaona, Shahidi wa Utetezi anayo haki kumwita shahidi, kwa sababu zamu ya mwendesha mashtaka, alimwita shahidi. Sasa Shahidi wa Utetezi atamwita shahidi. Naye Shahidi wa Utetezi anataka

kuwasilisha kwa mahakama hii, alasiri ya leo, nabii Nuhu. “Njoo huku mbele, Nuhu, ukachukue nafasi. Sasa, nasikia ya kwamba unayo ushuhuda kuhusu Neno la Mungu ambalo ulipewa.”

“Ndiyo.”

³⁸ Shahidi leo hii anataka kusema, kwa mahakama hii, ya kwamba yeye alikuwa ni mtu wa kawaida tu naye alimwamini Mungu. Naye aliishi katika wakati wa kisayansi, ambapo waliamini kwamba siku za miujiza hazikuwepo kamwe. Hakukuwahi kuwepo mvua juu ya ardhi, lakini siku moja alikutana na Mungu. Ndipo Mungu akamwambia aitengeneze safina kwa ajili ya kuwaokoa watu, na wote watakaoingia ndani ya hii safina watakokolewa. Naye Shahidi anataka kusema ya kwamba yeye kwa heshima, kwa moyo wake wote, aliamini Hilo. Ndipo akaanza kuhubiri Hilo. Basi akaenda, sio tu kulihubiri, bali, kufanya ninii zake—kazi zake zishuhudie imani yake, alianza kuijenga safina.

³⁹ Basi shahidi anataka kuelekeza kidole kwa Bw. Asiyeamini, na kwa Bw. Mwenye Kushuku, na Bw. Mkosa Subira. “Walinisumbua mchana na usiku. ‘Mvua hiyo itanyesha lini? Aha, ulisema hilo mwaka mmoja uliopita, na hakuna mvua huko juu. Tumewaendea wanasayansi nao wakathibitisha hakuna mvua huko juu.’ Nao wakadai kuwa nilikuwa mwendawazimu. Pia walinidhihaki na kuniambia kwamba kwa jumla mimi nilikuwa ‘mjinga na punguani’ kuamini ahadi ya kijinga kama hiyo, kinyume na utafiti wa kisayansi.” Lakini akasema, “Niliendelea kufanya kazi kwenye mradi huo, kwa sababu, nilisimama imara kwa sababu nilijua ni Neno la Mungu Nalo haliwezi kushindwa. Nikaijenga safina.

⁴⁰ “Na baada ya safina kukamilika, ndipo wenye kudhihaki wakakimbia wakizunguka na kuzunguka safina, kila siku, niliposimama kwenye, mlango nikiwahubiria. Nao bado walisema, ‘Sasa, hiyo imekuwa ni miaka mia moja na ishirini iliyopita, sasa iko wapi mvua yako? Kwa hiyo, unaona, kazi yako yote ni bure,’ wakasema. ‘Wanasayansi wetu wako sahihi, na hakuna kitu kama hicho. Na wewe ni mzee punguani kwa kuamini ahadi ya kijinga kama hiyo.’

⁴¹ “Ndipo basi siku ikaja nilipoanza kuondoka asubuhi moja, kutoka katika safina yangu. Na, ghafula, bila mkono juu yake, mlango ukafunga moja kwa moja usoni mwangu, nami nikatiwa muhuri ndani. ‘Sasa ni nini kilichotendeka?’ Ndipo nikapanda ngazi nilizokuwa nimejenga, nikapanda juu kwenye kilele, na kufungua dirisha. Nami ningeweza kuwasikia huko nje; Bw. Asiyeamini akiwa ameketi kule, Bw. Mwenye Kushuku, na Bw. Mkosa Subira; wakisema, ‘Sasa kumetukia nini? Amejitenga mwenyewe!’ Ndipo nikafikiria hakika mvua ingenyesha wakati huo. Na siku nilipoingia ndani ilikuwa tarehe 27... ama siku ya 17 ya Mei. Mlango ulifungika usoni mwangu. Niliwaita watu wangu pamoja, kisha nikasema, ‘Iweni tayari, mvua

itakuwa ikinyesha katika dakika chache zijazo.' Na, kwa siku nzima, Bw. Asiyeamini na Bw. Mwenye Kushuku na Bw. Mkosa Subira wakatembea kuzunguka na kuzunguka safina yangu, wakinikosoa, wakisema kila aina ya uovu kunihusu. Lakini nililiambia kusanyiko langu, 'Iweni kimya. Mungu alitoa ahadi!'

⁴² "Siku ya pili, jua likachomoka, angavu; hakuna mvua, hakuna ngurumo, na hakuna radi. Siku ya tatu, vivyo hivyo, ya nne, tano, sita. Lakini asubuhi ya siku ya 24 ya Mei (miaka mia moja na ishirini baadaye), kukaja bubujiko likishuka toka Mbinguni. Na wote waliotiwa upako na Bw. Mwenye Kushuku, Asiyeamini na Bw. -subira wakaangamia nje."

⁴³ Shahidi wa Utetezi akasema, "Shuka chini, Nuhu. Ninataka kumwita shahidi mwingine. Njoo huku juu, Bw. Ibrahimu, ninataka utoe ushuhuda."

⁴⁴ Bw. Ibrahimu anainuka, na kusema, "Nilikuwa nikifanya kazi shambani mwangu nje tu ya Uru, nchi ya Wakaldayo. Nami nilikuwa nimemwoa dada yangu wa kambo, jina lake liliitwa Sarai nami jina langu lilikuwa Abram. Ndipo nikakutana na Mungu, na Mungu akaniambia kwamba nitakuwa na mtoto kupitia Sara. Naye Sara, wakati huu, alikuwa na umri wa miaka sitini na mitano, nami nilikuwa na umri wa miaka sabini na mitano. Ndipo Mungu akaniambia kwamba ningepata mtoto kupitia Sara, na kupitia mtoto huyo ulimwengu wote utabarikiwa, nami nitakuwa baba wa mataifa. Upesi nikarudi, kwa sababu ya furaha hii iliyokuwa moyoni mwangu. Daima nilikuwa ninawapenda watoto, na nikafikiria sitawahi kuwa na mtoto. Lakini Mungu aliposema kuwa nitampata, nilimwamini. Nilienda kwa daktari kufanya maandalizi. Akanifukuza kutoka ofisini, Bw. Asiyeamini alikuwa ameketi mle. Ndipo nikatoka nikaingia barabarani, nao watawala walitaka kunitia mbaroni kuwa ni wazimu. Halafu basi miaka ilipoendelea, Bw. Mkosa Subira alinitesa mchana na usiku.

⁴⁵ "Mwezi wa kwanza, nilimwambia mke wangu, Sara. Mnaona, alikuwa amepita kwa mbali wakati wa kukoma hedhi, alikoma katika kile kilicho kawaida ya wanawake. Kisha nikamwambia Sara, 'Mpenzi, tumeweka tayari vijibuti vyote na nguo zote za madoadao, na pi—pi—pini? Tumejitayarisha kikamilifu, sivyo?' 'Ndiyo, tumejitayarisha kikamilifu.' 'Itatendeka sasa, wewe tazama.' Na mwishoni mwa siku ishirini na nane, nikasema, 'Unajisikiaje mpenzi?' 'Hamna tofauti, Ibrahimu.'" Vema, alisema, "Nikasema, 'Mungu abarikiwe! Sara, usilitilie shaka. Mungu alisema hivyo, tutampata haidhuru!' Hii iliendelea kwa miaka.

⁴⁶ "Na baada ya mwaka baada ya mwaka kupita, Bw. Mwenye Kushuku, Bw. Asiyeamini, wote wakanidhihaki. Lakini katika miaka ishirini na mitano baadaye, huyo mtoto mchanga alizaliwa nikiwa na umri wa miaka mia moja. Mungu hakuniambia nitampata mtoto huyo siku iliyofuata. Alisema

nitampata! Nami sijali ilichukua muda mrefu kiasi gani, Mungu aliahidi! Nilingojea miaka ishirini na mitano. Walifikiri nitazeeka sana na kufariki, bali nikasema, ‘Siwezi kufa, ahadi ni kwa ajili yangu. Mungu alisema hivyo!’

47 “Bw. Mwenye Kudhihaki na Bw. Asiyeamini, Bw. Mwenye Kushuku, Bw. Mkosa Subira, daima walikuja karibu, wakawatia watu upako, wakasema, ‘Ibrahimu, ni watoto wangapi sasa, *baba wa mataifa*, ulio nao?’ Bali nilisimama imara, kwa maana sikusitasita kwenye Neno la Mungu kwa kutokuamini. Nilijua Mungu aliweza kutimiza kila Neno aliloahidi. Sikuangalia mwili wangu mwenyewe, japo ulikuwa umekufa, na kufa kwa tumbo la uzazi la Sara. Bali nilimwamini Mungu. Wakasema, ‘Vema, nilidhani ulisema miaka ishirini na mitano iliyopita ulikuwa uwe na mtoto mchanga?’ ‘Nilisema hilo miaka ishirini na mitano iliyopita.’ Lakini Bw. Mkosa Subira pale, alisema, ‘Vema, miaka ishirini na mitano imepita. Hebu jiangalie sasa! Ndevu za mashavuni zinaning’inia kufikia magotini mwako, karibu. Tazama, wewe ni mzee.’ Nilimjulisha kwamba Mungu hakuniambia ni lini nitakapompata huyu mtoto mchanga. Yeye alisema, ‘Utampata kupitia Sara,’ na hilo tosha! Nilisimama imara. Sasa Neno halikusema *lini*, lilisema itakuwa hivyo!”

48 Hebu tumwite shahidi mwingine upesi sana, hatuna muda mwingi. Tunaweza kuwaita mamia ya hao. Hebu tumwite shahidi mwingine tena, Musa, apate kushuhudia.

49 “Mbona,” akasema, “Nilifunzwa katika hekima yote ya Wamisri. Nilikuwa profesa kwa wale wasioweza kuwa nayo. Lakini siku moja nyuma ya jangwa, baada ya mimi kuwa na umri wa miaka themanini, nilikutana na Mungu. Na Yeye alikuwa katika umbo la ninii—la ishara, na Yeye alikuwa ni moto unaowaka huko nyuma kwenye kichaka. Ndipo Yeye—Yeye akaniambia kwamba alisikia kuugua kwa watu Wake, Naye alikumbuka ahadi Yake kuwakomboa. Ndipo akasema, ‘Ninakutuma.’ Nami nikasema, ‘Mimi ni nani? Siwezi kwenenda vizuri. Mimi—mimi—mimi si—mimi si ninii—mimi si mwanathiolojia. Si—siwezi kwenda.’ Yeye akasema, ‘Utapewa ishara mbili. Moja ya hizo itakuwa katika mkono wako, nyingine itakuwa kwa fimbo. Na iwapo hawatasikia sauti za ishara hii, basi mwaga maji juu ya ardhi, yatageuka kuwa damu, basi hilo latosha.’

50 “Nilipochukua ishara yangu aliyonipa Mungu na kushuka kwenda mbele za Farao, Mchungaji Farao, alijaribu kuifanya karama yangu kuonekana kama kitu cha udanganyifu. Alisema, ‘Karibu kila mpiga ramli wa kawaida au Mmisri anaweza kufanya hayo. Karibu kila mchawi wa kawaida anaweza kufanya haya mazingaombwe.’ Basi akawatoa jamaa wawili wanaoitwa Yambre na Yane, na kwa kweli waliiga kila kitu nilichofanya. Lakini hilo halikunikomesha, kwa sababu ile Sauti

iliyonituma ilikuwa Sauti ya Kimaandiko, nami nilidumu nayo. Ilikuwa ni Neno la Mungu.

⁵¹ “Ilikuwa ni ishara ya Kimaandiko na Sauti ya Kimaandiko, ‘Kwa kuwa nakumbuka ahadi Yangu, na wakati umewadia.’ Hawakuwa wamekuwa na manabii Israeli kwa mamia ya miaka, miaka mia nne na arobaini, hawakuwa na manabii Israeli. Lakini Yeye alisema, ‘Ninakutuma uwe mmoja.’” Kisha akaenda. “Ndipo akaniambia kwamba, kwa ishara, ‘nitarudi na kuwaleta watoto kwenye mlima huu.’ Ilichukua muda mrefu, lakini niliwaleta. Nilidumu mwaminifu kwa Neno. Na wakati Yambre na wale waigaji wa kimwili waliojaribu kuidhihaki, hata hivyo nilijua haijalishi ni dhahaka kiasi gani wangeweza kutoa . . .”

⁵² Je! mwajua ya kwamba hayo yanapaswa kujirudia tena katika siku za mwisho? Yesu alisema hivyo. Biblia ilisema, “Kama vile Yane na Yambre walivyompinga Musa, ndivyo watakvayofanya watu hawa katika siku za mwisho,” waigaji wakijaribu kuigiza, kufuatisha.

⁵³ Bali alisema, “Nilisimama kimya kwa sababu nilijua ile Sauti ilikuwa ni Sauti ya Kimaandiko.” Japo kulikuwa na wawili wao, na yeye mmoja tu. Lakini alishuka akafanya kile yeye . . . naye, ilithibitika kuwa kweli, alirudi moja kwa moja kwenye mlima ambapo Mungu alimwambia.

⁵⁴ “Shuka chini, Musa. Hebu na tumwite shahidi mwingine upesi sana. Yoshua.”

⁵⁵ Yoshua akasema, “Tulipokuwa tunaikaribia nchi hiyo, tulifika Kadesh-barnea. Ndipo Musa, mtumishi wa Mungu, alienda akachukua nanii wote . . . mmoja kutoka kila kabila, mmoja kutoka kila dhehebu, ndipo akasema, ‘Hebu tuvuke twende tukaipeleleze nchi hiyo.’ Basi tukavuka, sisi wawili, na tukaleta ushahidi kwamba nchi hiyo ilikuwa nzuri.” Walikuwa na ushahidi wake. Hao walikuwa Wapentekoste halisi. “Kwa hiyo wakarudi pamoja na ushahidi kwamba nchi hiyo ilikuwa nzuri. Lakini ilipofikia kuichukua nchi yote, walisema, ‘Hatuwezi. Hatuwezi. Hatuna uwezo.’ Na watu walivurugika kabisa, hawakujua la kufanya, ni shirika gani la kuendea. Ndipo nikawatuliza, nikasema, ‘Kumbukeni, ni ahadi ya Mungu! Mungu alisema, “Nimewapa nchi hii.” Na kile anachoahidi Mungu, atafanya!’ Nikawatuliza watu. Kesho yake, unasema, ‘Hivi tutaondoka?’ Siku iliyofuata, ‘Tutaondoka?’ Ilikuwa ni miaka arobaini baadaye, bali tuliichukua nchi hiyo!”

⁵⁶ Shahidi mmoja zaidi, upesi sana, hebu nimwite Isaya kizimbani. “Isaya, waweza kushuhudia kwa ajili ya Shahidi wa Utetezi, na utupe utetezi kwa ajili ya washtakiwa, Mshtakiwa?”

⁵⁷ “Nitashuhudia. Nilikuwa nabii. Nilikuwa nabii aliyethibitishwa. Niliyosema, hayakuwa ninii . . . Si—sikujuu niliyokuwa nikisema, lakini Mungu alifanya niliyosema kutimia. Kila mtu akaanza kuliadini, kanisa lote, walianza kuliadini.

Ndipo siku moja jambo lisilo kawaida likatukia. Bwana Mungu aliniambia, 'Israeli wanatafuta ishara, kwa hiyo nataka wafanye hivyo, bali nitawapa Ishara kuu. Na hiyo itakuwa kwa ajili ya wakati mkuu, wakati watakuwa na maduka makuu na jeti kuu na kuu, kila kitu kikuu. Nitawapa Ishara kuu, bikira atachukua mimba!' Na mimi nikiwa ni nabii aliyethibitishwa, kila bikira mdogo aliweka vijibuti vyake tayari, na kila kitu kingine, alikuwa 'atamzaa mtoto huyo,' naam, bwana, yeye alikuwa 'ndiye yule Yehova alimwita.' Kila namna ya mambo yaliendelea. Naam, bwana. 'Vema, sasa, tunamtarajia, binti yangu, achukue mimba.' Huyu alifikiri ni *huyu*; kila msichana alikuwa anatazamia jambo hili. Miaka ikapita. Baadhi yao wakajikuna kichwa, kasema, 'Yule mzee nabii bandia.' Bali ilikuwa ni miaka mia nane baadaye. Hakusema ni *lini* atakapochukua mimba, Yeye alisema atachukua mimba! Miaka mia nane baadaye bikira akachukua mimba."

⁵⁸ Sasa kwa ajili ya ushuhuda wa mwisho, kama mtaniwia radhi, je! naweza kuwa shahidi wa mwisho? Hiyo si huko nyuma katika Biblia, hiyo ni sasa. Hebu niwe shahidi anayefuata, kwa dakika chache tu kabla hatujaanzisha mstari wa maombi. Basi sikilizeni kwa makini. Ningependa kutoa ushuhuda kwa ajili Yake. Ningependa niitwe kizimbani, kisha niinue mkono wangu kusema Kweli, si chochote ila Kweli.

⁵⁹ Ningependa kusema, nilipataje kuwa Mkristo? Baba yangu na mama, babu, nyanya, pande zote mbili, wote walikuwa wenye dhambi. Na asili yangu ilikuwa ni gugu... basi ikiwa nitakuwa punje ya ngano. Lakini asubuhi moja katika maskini kibanda cha magogo huko chini Kentucky, ndivyo walivyosema mamangu na mkunga, mnamo tarehe 6 Aprili, saa kumi na moja asubuhi, 1909, wakati Bwana Mungu aliponileta duniani, kulikuwako na Nuru iliyotulia kwenye kidirisha kidogo. Ndipo walipolivuta na kulifungua dirisha, mama akiwa amelala kwenye maskini kijitanda duni, aweze kuona ni mtoto wa aina gani aliyemzaa, Nuru ikaja ikizunguka na kuingia. Nao watu wa milimani hawakujua cha kuwazia kuhusu Hiyo. Nilikuwa mdogo sana kuweza kujua hii.

⁶⁰ Na kama mtoto, yapata umri wa miaka minane, umri wa miaka saba au minane, nilikuwa nikiteka maji kupeleka katika kikeneko cha pombe haramu cha babangu. Na wakati alasiri moja yenye joto ya Septemba, huku nimeketi chini, nikilia, nikienda nje kuvua samaki kwenye kidimbwi pamoja na wavulana, na wao... nisingeweza kwenda kwa sababu ilinibidi kuyapeleka maji haya. Nilisikia kama Upepo wa Kisulisuli katika mti, karibu nusu urefu wa kwenda juu. Kimya, kila mahali pengine, Septemba huko Indiana, kila kitu kimetulia, kinakufa, kimya. Na huu Upepo wa Kisulisuli kwenye kichaka, kukaja Sauti kutoka pale, na ikasema, "Kamwe usivute sigara, kunywa pombe, kuchafua mwili wako (huko ni

kutembea na wanawake), chochote kama hicho, kwani kuna kazi utakayofanya utakapokuwa mkubwa.” Ndipo mamangu akamwita daktari, alidhani nilikuwa na wasiwasi sana.

⁶¹ Wiki moja baadaye, nililiona Daraja la Manispaa, katika mpagao, nilivyouta, nililiona Daraja la Manispaa likikingama Mto Ohio, nikaona watu kumi na sita wakipoteza maisha yao katika hilo. Miaka ishirini na miwili kuanzia siku hiyo, Daraja la Manispaa linakingama mahali pale pale, na watu kumi na sita wakapoteza maisha yao katika hilo.

⁶² Katika Kinu cha Green usiku mmoja, bila kujua kuwa haya yote yalihusu nini. . . Baadaye nikawa mhudumu kumtumikia Bwana. Kwenye Kinu cha Green usiku mmoja. . . Ndiyo kwanza wachungaji wangu waniambie. . . Ningewaambia kuhusu kwenda, kuwa na ninii. . . kuwa na uwezo wa kuona mambo, nao wakaniambia ilikuwa ni ibilisi. Nami nikiwa ni Mkristo, sikutaka chochote kinachohusiana na ibilisi, hata kidogo. Kwa hiyo nikaenda kule juu, nikasema, “Bwana, siwezi kuachilia. . . kupitia maisha namna hii.” Na nikaketi huko juu nyuma kabisa kwenye kituo cha kuvulia samaki, nikiomba. Ndipo usiku mmoja hapo, kama Bwana alivyokuwa ameninenea, na katika mti, kama alivyomfanyia Musa. Basi hapa katika Kinu cha Green, kulikuja Mtu akaingia na kuniambia kwamba, nisijaribu kuomba kuondolewa Hii, bali ilikuwa ni karama iliyotumwa kutoka kwa Mungu, iliyokuwa ipelekewe watu wa ulimwenguni, na kunifanya nijue kupitia Maandiko ya kwamba mambo haya yote yaliyokuwa yameahidiwa kulingana na Biblia lazima yatimie, kwamba wakati ulikuwa umewadia.

⁶³ Ndipo nikarudi na kumwambia mchungaji wangu. Nilishuka na kumwambia, naye akasema, “Billy, umekula nini? Uliota, je! hiyo ilikuwa ni jinamizi?” Bali, kwangu mimi, ilikuwa ni Malaki 4. Akasema, “Utafanyaje hilo?” Ilikuwa ni Luka 17:30. Pia ilikuwa ni Ufunuo 10. Pia ilikuwa ni Maandiko haya yote yaliyoahidiwa kwa ajili ya siku za mwisho. Sikuliona likitendwa moja kwa moja wakati huo. Watu walishangaa, “Hili litatukia lini?” Bali nilishikilia tu.

⁶⁴ Siku moja kwenye mto, nilikuwa nikibatiza watu mia tano kwenye mto, wakati, mara, Nuru ii hii iliyoingia wakati nilipokuwa mvlana mdogo. Nami nilikuwa nimewaambia watu nilikuwa nikiiona. Wakasema nilikuwa nikiota na ilikuwa ni namna fulani ya dhana ya kiakili niliyokuwa nayo. Lakini mbele za watu zaidi ya elfu tano, mnamo saa nane alasiri, katika mwaka wa 1933, kutoka angani kukaja Wingu hili likishuka, likinena Maneno haya, “Kama vile Yohana Mbatizaji alivyoagizwa kutangulia kuja kwa kwanza kwa Kristo, huduma yako itatangulia kuja kwa pili kwa Kristo,” ambapo maelfu mara maelfu ya watu walilisikia, nayo magazeti yakatoa ushuhuda wake.

⁶⁵ Ninataka kusema, na ninataka kuelekeza hili kwa usikivu wa huyo mwendesha mashtaka kipofu anayeangalia kote ili mtu fulani awe na alama za miiba na misumari, na kila kitu namna hiyo. Halisemi hivyo! Halitoi ahadi kama hiyo.

⁶⁶ Tunasoma hapa katika Luka, mlango wa 17 na kifungu cha 30, Yesu akizungumza, “Kama ilivyokuwa katika siku za Sodoma, ndivyo itakavyokuwa wakati atakapofunuliwa Mwana wa Adamu.” Wakati anapofunuliwa! Ninataka kuvuta usikivu wenu kwa hili kwa dakika chache tu, kama mtavumiliana nami dakika zingine chache tu sasa. Iweni na kicho kabisa kwa dakika chache tu.

⁶⁷ Tazameni, Yesu alibeba majina matatu; Mwana wa Adamu, Mwana wa Daudi, Mwana wa Mungu. Alikuwa na majina matatu. Yote mtu yule yule, bali akiwa na majina matatu. Kama tu vile Baba, Mwana, Roho Mtakatifu; yote Mungu yule yule, sifa tatu.

⁶⁸ Kama vile tu mimi. Mke wangu huniita mume. Watoto wangu hawana chochote kuhusiana nami kwa jina la mume, mimi ni baba yao. Mjukuu wangu mdogo anayeketi pale, hana chochote kuhusiana nami kwa jina la baba, si chochote kwa jina la mume, yeye ni mjukuu wangu. Na yote ni mtu yule yule.

⁶⁹ Ndipo tunatambua wakati Yesu alipokuja na kujaribu kujifunua Mwenyewe kama Mwana wa Adamu (usikose hili), wakati alipojifunua Mwenyewe na kujiita Mwenyewe, daima, “yule Mwana wa Adamu,” Israeli ilipofushwa. Hawakujua chochote kuhusu kile Mwana wa Adamu lilimaanisha. Bali walisema, “Mwana wa Daudi,” wakati Bartimayo kipofu alipotoka mbio na kumtambua. *Daudi* lilimaanisha “Mfalme.” Kumbukeni, Mwana wa Adamu, Mwana wa Daudi, Mwana wa Mungu (ambaye alikuwa ni Bwana). Myahudi huyu alipata alichoomba kwa maana alimwendea katika Jina la Mwana wa Daudi, Mfalme; hakuwa Mwokozi, bali alikuwa ni Mfalme.

⁷⁰ Lakini wakati yule mwanamke Myunani, Msirofoinike alipomwendea katika jina la Mwana wa Daudi, Yeye hata hakuinua kichwa Chake. Hakuwa na madai Kwake katika jina la Mwana wa Daudi. Yeye hakuwa Mwana wa Daudi kwa huyo mwanamke Msirofoinike. Bali aliposema, “Bwana,” hapo akageuka. Alikuwa ni Bwana. Mnaona? Bwana, Yeye alikuwa ni Bwana! Si Mwana wa Daudi kwake.

⁷¹ Sasa, ni kwa nini hakutambuliwa kama Mwana wa Adamu? Mwana wa Adamu ilikuwa ni ufunuo wa kiroho, nabii. *Mwana wa Adamu* maana yake ni “nabii.”

⁷² Sasa kama mtageukia kwenye Biblia zenu katika Ezekieli, mlango wa pili na kifungu cha kwanza, mtaona kwamba Ezekieli alikuwa nabii, Neno la Mungu kwa ajili ya siku hiyo. Na Yehova Mwenyewe alimwita mwana wa Adamu. Yehova alimwita mwanadamu, mwana wa Adamu, kama vile Yesu

alivyojifunua kama Mwana wa Adamu. Ilikuwa ni kitu gani? Neno lililoahidiwa la wakati huo likidhihirishwa, Mungu yule yule! Mungu wa wakati wa Ezekieli, Mungu wa wakati wa Yesu, Mwana wa Adamu! Yeye kwa wakati huo hakuwa . . .

⁷³ Alikuwa ni Mwana wa Adamu kwa sababu alikuwa amekuja kujifunua Mwenyewe kwa Israeli kama Nabii, nao wakaukataa. Na huo ulikuwa ndio unabii ambao kwao walipaswa kumpokea, katika jina la Mwana wa Adamu, Nabii, kwa sababu ilikuwa ni kulingana na Neno. Kumbukumbu La Torati 18:15, “Bwana Mungu wenu atawaondokeshea Nabii kama mimi.” Na wakati alipokuja, alijitambulisha Mwenyewe katika huduma Yake kama mwanadamu, si Mwana wa Mungu, Mwana wa Adamu! Mungu ni Roho. Na Yeye alijifunua Mwenyewe kama Mwana wa Adamu, kile alichodai kuwa. Na wao walipofushwa hata wasingeweza kuona hilo.

⁷⁴ Bali sasa kwa Wamataifa Yeye anajifunua Mwenyewe, na sasa Mwana wa Mungu ambaye ni Roho Mtakatifu. Sasa, Yesu alisema, “Kama ilivyokuwa katika siku za Sodoma!”

⁷⁵ Ninamtaka huyu mwendesha mashtaka kipofu aone hili. Yeye ni mfasiri kipofu wa Neno, daima. Yeye huchukua mawazo yake ya kidhehebu kuhusu Hilo, na hajui kuhusu Hilo zaidi ya chochote. Yeye hufanya hivyo ili kudanganya, kwa sababu yeye ni mdanganyifu hapo mwanzo.

⁷⁶ Yesu alisema, “Kama ilivyokuwa katika siku za Sodoma, wakati Mwana wa Adamu anapofunuliwa!” Katika siku za Sodoma ilikuwa ni Mwana (huyo alikuwa ni Mungu) akifunuliwa katika mwili wa mwanadamu, ambaye wakati mmoja aliitwa Melkizedeki, Baba. Melkizedeki wakati huo alikuwa hana baba wala mama, pia hana mwanzo wa siku Zake wala mwisho wa maisha; yeyote Yule ambaye alikuwa, anabaki yuyo huyo. Yesu alikuwa na baba na mama; lakini Mtu huyu alikuwa hana baba wala mama. Na Yeye alimtokea Ibrahimu katika umbo la Mwana wa Adamu, Elohimu, Yehova. Kanisa sasa limetumikia kipindi kupitia wakati wa kanisa, katika ubatizo wa Roho Mtakatifu. Lakini Yesu alisema hapa, kuifanya Malaki 4 na Maandiko haya mengine kuwa halisi kwenu, mnaona, kwamba “Katika siku za mwisho, kabla tu ya kule Kuja, hali ya ulimwengu itakuwa kama Sodoma, ndipo Mwana wa Adamu atajifunua Mwenyewe kama Mwana wa Adamu kama alivyofanya katika siku za Sodoma.”

⁷⁷ Mwendesha mashtaka kipofu, hivi huwezi kuona hilo? Maneno Yake ni kweli. Si makovu ya misumari na alama na miiba.

⁷⁸ Ni Mwana wa Mungu akiwakilishwa katika Kanisa Lake, kama Mwana wa Adamu. Haina budi kutimiza Malaki 4 na Maandiko hayo mengine. Ninataka usikivu wa mahakama, mwangalie hilo kwa makini sana, “Mwana wa Adamu”! Kama vile Mungu Baba, Mungu Mwana, Mungu Roho Mtakatifu; ni

Mungu yule yule, sifa tatu mbalimbali za Mungu yule yule. Sasa, hili ni Mwana wa Daudi. . . Mwana wa Adamu alifunuliwa wakati huo kama Nabii. Mwana wa Daudi, Mfalme. Na sasa Mwana wa Mungu kwa wakati wa kanisa, kama, Mungu si mwanadamu, Mungu ni Roho, na Mwana wa Roho ni Roho Mtakatifu, ambaye anafunua wakati wa kanisa. Bali imeahidiwa hapa, “Katika siku za mwisho, kwamba Mwana wa Adamu atakapofunuliwa”!

⁷⁹ Mwendesha mashtaka kipofu, unaelewa hiyo? Na ninataka ujue, ewe mwendesha mashtaka kipofu, tunalionga, tunaliadini, Maneno haya yakitimizwa mbele zetu na tunajua kwamba hayo ni Kweli.

⁸⁰ Kwa Mayahudi Yeye alikuwa ni Mwana wa Daudi. Kwa Wayunani alikuwa ni Bwana, kwetu Yeye ni Bwana, kwa Wamataifa. Na sasa katika siku za mwisho, atarudi tena kama Mwana wa Adamu, kwa sababu Malaki ameahidi kwamba kutakuwako nabii atakayeinuka katika siku za mwisho ambaye atairudisha mioyo ya watu irudi kwa (mbali na madhehebu) irudi kwa Neno la asili, Imani ya baba zetu, Pentekoste ya asili. Na wakati alipofanya hilo, Yohana Mtakatifu 14:12, kazi alizofanya Yeye zitafanywa pia. Ufunuo 10 iliahidi siri yote. Utazifunua siri? Kuona kile Luther alichocha, kuona kile Wesley alichocha, kuona kile Pentekoste ilichoacha, na kuifunua siri ya moyo, kumfanya kuwa Mungu yule yule kupitia kila wakati, ambalo si kitu ila Neno la Mungu likidhihirishwa kumrudia Mwana wa Adamu tena. Hatutazamii makovu ya msumari; tunatazamia Neno lililodhihirishwa. Tazama, Mungu aliahidi mambo haya sasa, na Yeye anayafanya kama tu alivyosema. Ningeweza kusema zaidi, bali, tutaliacha somo, kunachelewa.

⁸¹ Bw. Mwendesha Mashtaka, ninataka ufahamu kwamba ningeweza kuita maelfu ya mashahidi hapa alasiri hii. Ninataka ujue ya kwamba mambo aliyosema kuwa alifanya, sisi ni mashahidi kwamba “Yeye hutimiza Neno Lake!” Kuna mkutano wa Roho Mtakatifu halisi! Kuna nguvu halisi za Mungu! Na kuna ahadi halisi kwamba watapata afya, wakiweka mikono juu ya wagonjwa. Ninataka ujue hilo. Ninataka ujue alisema, “Kama ilivyokuwa katika siku za Sodoma, ndivyo itakavyokuwa katika kuja kwake Mwana wa Adamu.”

⁸² Mimi ni mgeni, nami ninashuhudia tu yale Biblia inayosema kuwa ni Kweli. Mkitambua, yule Malaika wa Bwana aliyekuja katika umbo la mwanadamu, alikuwa ameuelekeza mgongo Wake kwenye hema, Naye akamwambia Ibrahimu kile Sara alichokuwa akiwaza. Yesu alisema ingejirudia. Sasa, kama nimesema Kweli, hebu Mungu na athibitishe hilo kuwa ni Kweli. Hebu alifunue. Halafu, si siri, tunajua basi. Ninii. . . Nitaondoka kwenye mahakama hii alasiri ya leo na uamuzi huu, kuamua niani mwako mwenyewe. Hebu Mungu aliyetoa

ahadi... Si huko nyuma katika siku zilizopita; zilizithibitishwa. Hebu Mungu aliyetoka ahadi aithibitishe leo hii, aseme vile vile. Baadhi yenu tafakarini moyoni mwenu, mwombe Mungu kwa ajili ya ugonjwa wako au mateso yako, na uone ikiwa Mungu atafunua siri ya moyo. Nawapa changamoto mfanye hivyo, kutoka upande mmoja hadi mwingine. Sasa, je! ningethubutu kufanya jambo kama hilo kama sijasimama hasa juu ya yale Maandiko yasemayo? Ninaitaka mahakama hii ione kwamba ni Yeye yule jana, leo, na hata milele, kwamba Yeye hutimiza ahadi Yake. Naye aliahidi kwamba Yesu Kristo angefunuliwa katika siku za mwisho, kama Mwana wa Adamu. [Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.]

⁸³ Mtu anayeketi hapa akiugua bawasiri. Sijawahi kukuona maishani mwangu. Kama hiyo ni kweli, inua mkono wako. Unaniamini mimi kuwa nimetoa ushuhuda wa Neno la Mungu? Huyu ni mkeo anayeketi karibu na wewe. Anaugua pia, uvimbe kichwani mwake. Hiyo ni kweli, inua mkono wako. Unaamini Mungu anaweza kuniambia wewe ni nani? Kama angali ni Neno, Neno linajua siri za moyo. Nyinyi ni Bw. na Bibi Hunt. Ikiwa hiyo ni kweli, inua mkono wako. Kwa nini usiamini Hilo?

[Dada mmoja anaanza kunena katika lugha nyingine. Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.]

⁸⁴ Hapa, huyu hapa ameketi mwanaume anayeketi papa hapa, amekiinamisha kichwa chake, analia, akijiombea mwenyewe na pia kwa ajili ya mkewe. Mke hayupo hapa. Hayuko pamoja nawe alasiri ya leo. Anaugua. Unafikiri Mungu anaweza kuniambia shida yake ni nini, naye hayupo hapa? Unaamini? Unaamini? Mimi ni mgeni kwako, hiyo ni kweli? Mkeo ana ugonjwa wa kike. Kama hiyo ni kweli, inua mkono wako, juu, ili wauone. Na jina lako ni Bw. Smith. Unaamini kwamba Mungu atamponya? Kama hiyo ni kweli, punga mkono wako juu-na-chini, namna *hii*.

Nakupa changamoto kuamini kwamba Yesu Kristo amefunuliwa katika umbo la Mwana wa Adamu, katika mwili wa binadamu, kupitia Mwili wa Bibi Arusi. Kubali mwito Wake.

⁸⁵ Huyu hapa mwanamke ameketi hapa akiniangalia. Anaugua presha ya juu ya damu. Unaamini kwamba Mungu anaweza kuniambia kuwa wewe ni nani? Unaitwa Daisy. Kama ukininii... Je! hiyo ni kweli? Inua mkono wako. Amini sasa kwa moyo wako wote, Yesu Kristo atakufanya... atakupa haja yako. Unaona, ni Yeye yule jana, leo, na hata milele. Unaamini hilo?

⁸⁶ Huyu hapa mwanaume anayeketi moja kwa moja hapa nyuma akiniangalia, anao mzigo moyoni mwake. Ni kwa ajili ya mwanawe, mwanawe ana kisukari. Je! unaamini? Huyu ni mkeo aliyeanza kulia moja kwa moja karibu na wewe hapo, anao mzigo moyoni mwake. Huo ni kwa ajili ya dadake. Dadake ana ugonjwa wa moyo, tatizo. Nyinyi ni Bw. na Bibi Sickles.

Kama hiyo ni kweli, pungu mkono wako juu chini namna *hii*. Ikiwa mimi ni mgeni kabisa kwenu, simameni kwa miguu yenu. Simameni, ikiwa mimi ni mgeni kwenu na siwajui.

⁸⁷ Ni kitu gani? Kutimizwa kwa Neno la Mungu katika siku za mwisho! Mwendesha mashtaka, nataka ufahamu ya kwamba Neno la Mungu ni kweli. Mungu aliniambia hilo miaka thelathini na mitatu iliyopita. Nimesubiri muda huu wote, bali limetimia papa hapa alasiri ya leo. Mungu hutimiza Neno Lake! Ni Yeye yule jana, leo, na hata milele. Mungu akubariki; nenda ukapate shauku yako sasa.

⁸⁸ Nia yako ndiyo wazee wa mahakama. Wazee wa mahakama hawana budi kufanya uamuzi. Na jinsi unavyotenda kuanzia sasa na kendelea itatangaza au kuonyesha watu uamuzi wako. Hivi Yeye ana hatia au hana hatia? Je! unaamini kwamba Yeye hana hatia, kwamba Yeye hutimiza Neno Lake? Ni sisi tulio na ninii... Tunamsikiliza mzee Mkosa Subira, Bw. Asiyeamini, na Bw. Mwenye Kushuku. Lakini sasa je! mtaamini ya kwamba Mungu hutimiza Neno Lake? Nia yako ndiyo wazee wa mahakama. Na jinsi unavyotenda tangu sasa na kuendelea itathibitishia watu kilicho uamuzi wako. Mnaamini hilo? Hebu na tuinamishe vichwa vyetu basi.

⁸⁹ Nimewaambieni Kweli halisi. Iwapo tungekuwa na wakati kukaa hapo, hakuna Andiko moja katika Biblia ila lile litakaloshuhudia jambo lilo hilo. Nimekuwa mnyofu. Mnajua, wakati mwingine, kuwa mnyofu si kazi rahisi. Bali mradi tu Mungu amesimama pale! Haikuwa rahisi kwa Luther, Wesley, wala hata mmoja wa wale wengine. Si rahisi kwako au mtu yeyote mwingine anayechukua msimamo. Lakini alasiri ya leo huna budi kuchukua msimamo wako. Yeye kamwe hakusema... Alisema, "Wataweka mikono juu ya wagonjwa, nao watapata afya." Ukiamini hilo, basi sijali kama linatendeka papa hapa, kama likitendeka juma lijalo, likitendeka miaka ishirini kuanzia leo; kama ukiliamini kikamilifu, litatendeka. Mimi...

⁹⁰ Yupo daktari aliyeketi hapa sasa, ninavyosikia. Ninataka kumshukuru. Nilikuwa kwa mgonjwa, kumwona mgonjwa wake, muda mfupi uliopita, mapema asubuhi ya leo katika hospitali, aliyekuwa yuafa, ndivyo wanavyofikiri. Ameliwa sana na kansa. Ndipo maskini mwanamke huyu akaniambia, kasema, "Daktari wangu wa upasuaji amekuwa akihudhuria mikutano yako, naye anakubaliana nawe. Na siyo hiyo tu, bali, Ndugu Branham, ninataka ufahamu anasimama nawe katika maombi kwa ajili yangu." Kama ningehitaji huduma yoyote ya tiba, ningetaka yeye anihudumie, mtu awezaye kumtumainia Mungu namna hiyo! Naam. Wako katika kila sehemu ya maisha, katika taaluma zote.

Hebu tukumbuke, uamuzi ni wako sasa.

⁹¹ Bwana Yesu, nimejaribu tu kueleza Neno. Umeshuhudia kwamba ni Kweli. Mashahidi Wako, tungeweza kuwaita mamia, na hata hivyo hatuna muda. Hapa pia zipo lesu, zimewekwa hapa, zinazowaendea wagonjwa na wanaoteseka, papa hapa ambapo Roho Mtakatifu anatoa ushuhuda kwamba Yesu angali hai. Tunamjua kwa Maisha Yake, maisha aliyoishi, mambo aliyofanya. Nasi tunaomba, Mungu, sasa tukiweka mikono juu ya lesu hizi, kwamba yeyote zitakayemgusa na waponywe. Ninatoa maombi yangu, kwa imani, pamoja na kundi hili lingine la waaminio, kwa ajili ya hawa ambao hawawezi kuwa hapa. Jalia waufurahie ukuu wa Mungu. Huenda ni wagonjwa na hawawezi kuja. Maskini baba fulani mzee aliyeketi huko nyuma chumbani, akigogota kwenye maskini fimbo nyeupe, alasiri ya leo, akiingojea lesu hii irudi. Yule mtoto aliyelala pale hospitalini, akiumia kwa joto la homa, na mtu fulani akingojea kumlelea lesu. Jalia nguvu za Mwenyezi Mungu ziende pamoja nazo, zitie upako kwa upako ule ule ambao umekuwaga juu ya mkutano alasiri ya leo. Na jalia wapone, Bwana. Tunafanya maombi haya kwa niaba yao, kwa kuwa hawakuwepo. Bali Wewe uko kila mahali. Naomba uwe hapo kuthibitisha Neno Lako, kupitia Jina la Yesu Kristo.

⁹² Sasa jalia Roho Mtakatifu kwa kweli, si mhemko fulani, si namna fulani tu ya matumaini nusunusu, bali uamuzi wa kweli na ufanywe kwa ajili ya hii, kile ninachokiita alasiri ya leo, “mahakama.” Jalia kila mmoja wao atoe ushuhuda vivyo hivyo, wakati wakichukua kadi yao ya maombi na kuishikilia mikononi mwao, wanapopitia mimbarani. Jalia, wakisha kuninii... wakihudumiwa kulingana na mlango wa 16 wa Marko Mtakatifu, “Wataweka mikono yao juu ya wagonjwa, nao watapata afya.” Wakati mtumishi Wako mteule anaposimama hapa na tunaweka mikono yetu juu yao, Bwana, jalia iumalize kabisa. Jalia watoke hapa wakiwa na furaha kabisa, na kusahau kuhusu kwamba waliwahi kuwa na shida zozote, kwa sababu wana hakika, kama Ibrahimu alivyokuwa, kwamba Mungu anaweza kutimiza ahadi alizofanya. Tunaomba katika Jina la Yesu. Amina.

Nampenda, nampenda
 Kwani alinipenda kwanza
 Na kununua wokovu wangu
 Mtini Kalvari.

⁹³ Ni wangapi mlio na uamuzi wenu? Inua mkono wako, “ninao uamuzi wangu.” Vema, mahakama, mtahudumiwa kulingana na Neno Takatifu la Mungu, “Ishara hizi zitafuatana na hao waaminio.” Sitawaacha mkiwa mmekeki hapa, mkidhani kwamba kwa sababu tu karama hii, kwamba hiyo inamfanya mtu yeyote chochote zaidi ya yeyote mwingine. Mnao wachungaji watauwa hapa. Wapo hapa, tutawauliza kusimama pamoja nami jukwaani. Wao watawawekea mikono yao kama

nifanyavyo mimi. Walitualika kuja hapa na wapo hapa kama ninii wenu...kama mashahidi wa Mungu. Wanatoa shuhuda kwa ajili ya ile Kweli. Sasa, hamwezi kusema, “Ndugu Branham aliweka mikono,” maana mikono yangu si zaidi ya yao au ya mwingine yeyote. Ni imani yako, uamuzi wako uliofanya juu ya Neno la Mungu. Mungu hutimiza! Na kama Mungu anaweza kutimiza sehemu hiyo ya Neno na kulithibitisha kwako, basi umeponywa tayari, kwa sababu kwa kupigwa Kwake uliponywa.

⁹⁴ Sasa, ninawataka wote walio katika sehemu *hii* hapa, walio na kadi za maombi, simameni upande huo karibu na ukuta. Sasa, nyote mlio katika sehemu *hii* hapa, mlio na kadi za maombi, simameni katikati ya marefu na muangalie nyuma kule. Na wote mlio katika sehemu *hii* hapa, mlio na kadi za maombi... Sasa, kwenye sehemu *hii*—*hii hapa*, sasa geukeni upande ule mwingine sasa, rudini nyuma hivi. Geukeni upande ule mwingine, maana ninataka mstari ulionyooka. Nyote mlio kwenye sehemu *hii*, tokeni huku, mwangalie nyuma kule. Na nyote mlio katika sehemu *hii* hapa juu, mlio na kadi za maombi, njoni upande huu na mwangalie nyuma upande ule, na mstari wa maombi utakuwa unaendelea. Wote walio kwenye roshani, na kadi za maombi, wanaotaka kuombewa, shukeni moja kwa moja na mjipange moja kwa moja nyuma ya sehemu *hii* nyingine wanapokuja. Huku wakija, ni... .

⁹⁵ [Ndugu Branham anazungumza na wahudumu kwenye jukwaa—Mh.] Mnataka niwaite wahudumu wengine? Je! ni sawa kutoa ushahidi? Nyote, je! ni sawa kwenu nyote? *Uamuzi* wako ni nini katika kesi? [Ndugu huyo anajibu, “Ninajua kwamba mambo hayo ni Kweli.”] Vema.

⁹⁶ Wachungaji wanataka kujua, wanautaka ushirika na wahudumu wengine. Wanamtaka mhudumu yeyote humu ndani anayemwamini Mungu, na anaamini kwamba kuweka mikono juu ya wagonjwa, ikiwa uamuzi wao alasiri ya leo, kwamba ni “Kweli,” wanawaalikeneni kama wenzi wao mje hapa na kusimama jukwaani pamoja nasi wakati tukiomba. Wachungaji wote waliojazwa na Roho wa Mungu, na uamuzi wenu sasa ni kwamba mnaamini kwamba ni Yeye yule jana, leo, na hata milele, mnaamini kwamba Marko 16 ni Kweli, wachungaji hawa hapa wanataka kuwaalikeneni hapa juu sasa kama wenzi wao kwa Injili. Njoni hapa juu na msimame kwenye jukwaa pamoja nasi wakati tunapofanya mistari *hii* ya maombi, kuomba. Papa hapa, waleteni huku juu. Wachungaji wote katika jengo, haijalishi dhehebu gani. Waliniambia tu niwaombe. Njoni hapa juu mkitaka kuja wakati huu, na mfanye mstari huu wa maombi kuombewa, kuombea wagonjwa, kuweka mikono juu ya wagonjwa.

⁹⁷ Ni wangapi humu ndani ambao si ninii...ni wazima, sasa, na haiwalazimu kuombewa, lakini ninyi ni waaminio, inua

mkono wako. Je! mtaniahidi pia kwamba maombi yenu yataenda juu pamoja na sisi wachungaji wakati tukiwaombea watu hawa? Vipi kama huyo alikuwa ni mama yako anayesimama pale? Vipi kama huyo alikuwa ni mke wako? Vipi kama huyo alikuwa ni ndugu yako ama dada? Kumbuka, ni mama wa mtu fulani, ni ndugu ya mtu fulani, ni dada ya mtu fulani, ni mvulana au msichana wa mama fulani, ni wa mtu fulani. Nasi tutawatendea wengine jinsi tungetaka wengine watutendee. Sasa, nawatakeni, kila mmoja kuwa na kicho na katika maombi.

⁹⁸ Na wakati karibu wamefanya mistari yao sasa, ambapo wanaweza kupitia, ninawataka wahudumu sasa waje hapa na kufanya mistari miwili moja kwa moja kupitia kando ya jukwaa hapa, moja kwa moja *huku* juu na kushuka hivi, fanyeni mistari miwili ili kwamba watu wanaopita. Nitaiweka maikrofoni hii nyuma, Bw. Borders atasimama hapa akiongoza kwa wimbo. Hiyo ni kweli, mistari miwili kwenda juu na kushuka *hivi*, ili watu...

⁹⁹ Sasa, kwa kila mmoja wenu anayesimama kwenye mstari, kuihakikisha maradufu kwa Shetani, mwendesha mashtaka, kwamba uamuzi wako umefanywa. Uamuzi wako umefanywa, kwamba unaamini kuwa Marko 16 ni Neno la Mungu, na ni Kweli, nawe unapitia mstari huu ili uwekewe mikono. Na tangu sasa na kuendelea, tendo lako litathibitisha kilicho uamuzi wako. Inua mkono wako, na useme, “ninamwahidi Mungu hilo.” Nyote mlio katika mstari huo.

¹⁰⁰ Sasa na tuombe. Baba yetu wa Mbinguni, ninii... watu hawa, alasiri ya leo, wameelezwa kama mahakama. Ninahisi, Bwana, umekuwa na ke—kesi halisi. Pilato hakukufanyia ifaayo. Alikuwa na mashahidi wa uongo. Bali Wewe uliwashinda hao mashahidi wa uongo. Sha—Shahidi wa Utetezi, Roho Mtakatifu alikuja kulithibitisha Neno mbele za watu. Umefanyiwa kesi ya haki. Nao watu wamefanya uamuzi wao, walipitisha hukumu, wanasema, nao wanapitia kuthibitishia ulimwengu kwamba wanaamini Neno Lako ni hivyo. Limefasiriwa vibaya. Baadhi yao wakisema, “Hebu nikuone ukifanya *hili*, hebu nikuone ukifanya *lile*.” Hilo si kulingana na Neno Lako. Neno lilisema, “Watapata afya.” Nasi tumewaleta mashahidi jukwaani, kuthibitisha kwamba hilo ndilo ulilosema. Wewe hufanya mambo kwa njia Yako Mwenyewe.

¹⁰¹ Sasa, ninaomba, Baba, kwamba Wewe utajalia baraka hizi alasiri ya leo kwa watu. Kama mtumishi wako, pamoja na watumishi Wako wengine wote, mamia yao hapa, tunatoa maombi yetu kwa ajili ya watu hawa. Watie upako wachungaji hawa wazuri, Bwana. Mwenye kushuku akipata kuja karibu, au asiyeamini, ama Bw. Mkosa Subira, au yeyote wa hao wakosoaji, wenye kudhihaki ambao wamekuwako kupitia kila wakati, wakija karibu na watu hawa, jalia mahakama hii alasiri ya leo ipaze sauti dhidi yake, ushuhuda wao. Kwa

Nuhu, kama ilivyokuwa katika siku za Nuhu, kama ilivyokuwa katika siku za Sodoma, zote mbili kuingia katika maangamizi. Jinsi walivyodhihaki na kufanya mzaha! Lakini haikuleta tofauti yoyote, waaminio walishikilia moja kwa moja kwenye Neno. Nasi tuko tayari kushikilia Neno alasiri ya leo, Baba. Ninajiunganisha mwenyewe na wachungaji Wako wengine hapa, kuweka mikono juu ya watu hawa, jalia nguvu za Mwenyezi Mungu, ambazo tunajua zipo sasa zikithibitisha Neno, zimponye kila mmoja wao. Kupitia Yesu Kristo Bwana wetu. Amina.

¹⁰² Ndugu Roy, kama utakuja jukwaani. Kila kichwa kimeinamishwa sasa, kila mtu akiomba na kuimba. Usipomba, imba *Amini Tu*. Wakati ukipita, amini tu, upite. Haijalishi kile usemachi au utendalo, hiyo ni juu yako. Ukitaka kupaza sauti, paza sauti. Na kama unataka kuondoka... Haijalishi ni nini, mwamini tu Mungu. Ondoka tu na useme, “Imetulia moyoni mwangu.” Kama tu ambavyo ikiwa ulienda kwenye kidimbwi kubatizwa. Hilo latosha, ukiliamini. Wewe ni mkristo mradi tu unaamini. Je! hiyo ni kweli? Na utapona mradi tu unaamini. Hebu na tuombe sote sasa. Vema, Ndugu Borders. [Ndugu Branham anaombea wagonjwa. Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.] Amini tu!

Hata twonane! Hata twonane!

Hata twonane miguuni pa Yesu;

Hata twonane! Hata twonane!

Mungu awe nanyi hata twonane tena!

¹⁰³ Ninahudumu Neno la Mungu kwenu. Katika Jina la Yesu Kristo, hebu kila mmoja wenu na apokee kile alichoomba. “Ukiuambia mlima huu, ‘ng’oka,’ wala usione shaka moyoni mwako, bali uamini kwamba uliyosema yatatimia, yatakuwa yako.” Mwombapo, aminini kwamba mnapokea mlichoomba, nanyi mtapewa. Ninahudumu katika Jina la Yesu Kristo. Ninaamini kwamba uamuzi wetu umefanywa na umepitishwa na matendo yetu yanathibitisha sasa kwamba tunaamini, na tunajua Yeye aliponya. Nisipowaona tena ng’ambo hii ya mto, nitakutana nanyi ng’ambo ile. Basi Roho Mtakatifu mkuu ambaye amekuwa Mgeni wetu juma hili, hapa pamoja nasi na ametuhudumia, Yeye atawashuhudia wakati huo kwamba nimewaambia Kweli. Hadi wakati huo:

Hata twonane! Hata twonane!

Mungu awe nanyi hata twonane tena!

Hebu tuinamishe vichwa vyetu sasa.

¹⁰⁴ Kimya sana na kwa utamu. [Ndugu Branham anaanza kuvumisha *Hata Twonane*—Mh.]

¹⁰⁵ Hebu mawimbi ya mauti yaondoke mbele zenu. Hebu Mungu wa Mbinguni, ambaye tuko katika Uwepo Wake, awadumishe salama hata tutakapoonana.

Mungu akubariki, ndugu. Ninakuthamini.



KESI SWA64-0419

(The Trial)

Ujumbe huu uliohubiriwa na Ndugu William Marrion Branham, ulihubiriwa hapo awali katika Kiingereza mnamo Jumapili alasiri, tarehe 19 Aprili, 1964, katika Ukumbi wa McKay huko Tampa, Florida, Marekani. Kila jitihada imefanywa kuuhamisha ujumbe huu wa sauti kutoka kwenye kanda ya sumaku iliyorekodiwa na kuchapishwa bila kufupishwa katika Kiingereza. Tafsiri hii ya Kiswahili ilichapishwa na kusambazwa na Voice Of God Recordings.

SWAHILI

©2018 VGR, ALL RIGHTS RESERVED

VOICE OF GOD RECORDINGS

P.O. Box 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.

www.branham.org

Ilani ya haki ya kunakili

Haki zote zimehifadhiwa. Kitabu hiki kinaweza kuchapishwa kwa matbaa ya nyumbani kwa matumizi ya kibinafsi ama kusambaza, bila malipo, kama chombo cha kuitangazia Injili ya Yesu Kristo. Kitabu hiki hakiwezi kikauzwa, kunakiliwa kwa wingi, kuwekwa kwenye mtandao, kuhifadhiwa kikatolewe tena, kufasiriwa katika lugha zingine ama kutumiwa kuomba fedha bila idhini halisi iliyoandikwa moja kwa moja kutoka Voice Of God Recordings®.

Kwa habari zaidi ama kwa vifaa zaidi, tafadhali wasiliana na:

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. Box 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org